ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32 Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50. Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
56.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
57.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
58. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
59.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
62.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
63.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
64.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
66.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
69.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
70.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Sita – Tarehe 22 Juni, 2012

(Kikao Kiliaanza Saa 3:00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Muhammed Mussa) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 195

Maadhimisho ya Mwaka wa Kiislamu

Mhe. Salim Abdalla Hamad (Kny Mhe. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:-

Katika mikutano mitano iliyopita ya Baraza nimekuwa naulizia juu ya maadhimisho ya mwaka wa Kiislamu. Jibu ambalo nimepewa mara zote ni kuwa Serikali bado inalishughulikia suala hilo. Mara ya mwisho nilijibiwa kuwa suala hilo sasa linashughulikiwa na Mhe. Makampo wa Pili wa Rais.

(a) Kama ni kweli suala hilo linashughulikiwa kwenye hatua ya Wizara yako, ushughulikiaje wake uko katika hatua gani hadi hivi sasa.

(b) Je Mhe. Waziri ni lini Waislamu wa Zanzibar wataanza kusherehekea mwaka wa Kiislamu rasmi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 195 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-
Mhe. Mwenyekiti, ni kweli suala hili limeletwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kutoka Wizara ya Katiba na Sheria. Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais inalifanyia kazi suala hili kwa umakini mkubwa na itatolewa taarifa kamili mara tu baada ya kupata maelekezo ya Serikali. Kwa hivi sasa tunawaomba Waislamu wote nchini kuendelea kusherehekea mwaka mpya wa Kiisalmu kama tulivyokuwa tukifanya kwa miaka mingi huko nyuma na kusubiri maamuzi ya suala hili kutoka serikalini.

Nam. 23

Tatizo la Upatikanaji wa Vitambulisho vya Ukaazi Zanzibar

Mhe. Hassan Hamad Omar – Aliuliza:-

Hivi sasa kuna baadhi ya Wazanzibari halisi ambao hukosa haki ya kumchagua Rais wa Zanzibar kwa kukosa Vitambulisho vya Mzanzibari na badala yake hupata haki ya kumchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ni sababu gani za msingi zinazosababisha Wananchi hao kutopewa vitambulisho hivyo kukosa haki hiyo ya kumchagua Rais wa Zanzibar na badala yake kupewa haki hiyo kumchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 23 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho Zanzibar inafanya kazi zake kwa kuzingatia Sheria Namb. 7/2005 na Kanuni zake. Imewekwa wazi kila Mzanzibari Mkaazi alietimiza masharti anayo haki ya kupatiwa kitambulisho bila ya usumbufu wowote.

Mhe. Mwenyekiti, kwa wale ambao wana malalamiko ya kutopatiwa vitambulisho, Sheria hii imetoa mwongozo wa kukata rufaa kwa Mkurugenzi wa Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho, hakuna Mzanzibari Mkaazi atakaenyimwa haki ya kupewa kitambulisho iwapo atakuwa ametimiza masharti ya kisheria.

Kwa wale Wazanzibari tulisema kwamba ni halisi ambao hukosa haki ya kumchagua Rais kwa kukosa vitambulisho vya Uzanzibari ni wazi kwamba hawakutimiza masharti yale ya ukaazi, ndio maana wananyimwa vitambulisho na ndio maana wananyimwa hiyo haki ya kupiga kura kumchagua Rais. Lakini anayetimiza masharti hakuna matatizo mambo yote yanakwenda kama taratibu zinavyoelekeza. Ahsante.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa kuwa kuna wananchi waliotimia umri wa miaka 60 mpaka 70 waliopiga kura mwaka 2000, na mwaka 2005 na watu hao kuanzia mwezi wa 8 au wa 9 waliitwa katika sehemu ya kilimo na vitambulisho vyao walivyopiga kura vikatobolewa pembeni, na wakiwa na matumaini kwamba wanaweza kuipata haki yao na hawana vyeti vya kuzaliwa, lakini katika chaguzi zilizopita walishiriki.

Je, mwananchi huyu ana matumaini gani kama ni haki yake ya Kizanzibari na yeye ataipata kuwa na Kitambulisho cha Uzanzibari ambacho ni jambo muhimu sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumshauri Mhe. Mwakilishi, tushirikiane tupange mimi na yeye twende huko katika eneo tulitafutie ufumbuzi hili tatizo. Kwa sababu kwenye utendaji mimi sikatai matatizo yapo na yanatokezea. La msingi taratibu zifuatwe. Juzi nafikiri nilieleza juzi kwamba matatizo mengi yanatokezea kwamba wale watu wanahama kutoka sehemu moja au nyengine hachukui barua ya Sheha.

Lakini pia kuna watu ambao wamefika sehemu ile wako nje tu, wanataka kuja pengine chini ya ile miezi 36 iliyowekwa lakini wanataka wapige kura na wapewe kitambulisho cha Mzanzibari. Hapo ndio penye matatizo.
Mimi namshauri Mheshimiwa kama nilivyosema kwamba unaweza ukakata rufaa kwa Mkurugenzi au kwa Waziri. Mimi nakuomba tukitoka hapa tupange tuende huko tutamchukua na Mkurugenzi wetu wa vitambulisho tukalifanyie upembuzi yakinifu hili suala tuliondoe kabisa.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Namuuliza Mhe. Waziri kwa kuwa vitambulisho vya Uzanzibari Mkaazi sasa hivi imekuwa ni muhimu kuliko kitu chochote kama huna kitambulisho huwezi kupata kazi, kama huna kitambulisho huwezi kutumiwa pesa na ukazipata, kama huna kitambulisho si Mzanzibari. Kama huna kitambulisho shughuli zote unaweza ukazikosa.

Kwa kuwa kuna Wazanzibari ambao ni Wazanzibari halisi kwa mfano kama wazee aliosema wa miaka 60 na zaidi, na kuna vijana ambao ni Wazanzibari halisi hajaondoka kwenda wala kurudi. Na kwa kuwa karibu sasa hivi kuna marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Zanzibar, na Vijana hao pamoja na wazee hao wana haki yao ya msingi kushiriki katika marekebisho ya Katiba ya Serikali ya Muungano.

(a) Je, kutowapa vitambulisho watu hawa kwa masharti haya yaliyopo hatuoni kama tunawanyima haki zao.

(b) Je, kama tunawanyima haki zao za msingi serikali itaandaa utaratibu upi maalum utakaokuwa mzuri ili usimnyime fursa Mzanzibari ili kila Mzanzibari apate haki yake ya msingi aweze kuchagua, kuchaguliwa na kupata mambo mengine ambayo kuwa ni haki yake msingi kupata, aweze kukopa benki na mambo mengine. Ni lini hasa Serikali itaandaa utaratibu mzuri zaidi ili kuwaondolea wananchi wetu masharti magumu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri naomba kusisitiza tena ni haki ya kila Mzanzibari kuwa na kitambulisho hiyo ni haki yake, na hiyo ndiyo itakayomuwezesha kupata huduma nyingi kama ulivyosema. Kwanza usalama wake yeye mwenyewe, benki siku hizi mote kila unapokwenda unatakiwa uwe na kitambulisho cha Uzanzibari. Kukipata tunasisitiza kwamba tufate masharti yaliyopo, hapingwi mtu. Tatizo linatokezea kwamba masharti tunayakiuka.

Mhe. Subeit, mimi naomba nikariri Sheria hii hapa ya Sheria Nam. 7 ya mwaka 2005. Naomba niukariri kwa kizungu kidogo.

> *"The minister may make rules, orders, or regulations not inconsistent with the provision this act for the better carrying out the provisions of this act"*

Yaani mamlaka ya kufanya marekebisho na mengineyo. Mimi nashauri Mhe. Mwakilishi lete mawazo turekebishe sheria hii. Tunaamini yapo matatizo ya kiutendaji hatukatai, lakini tulete fikra twende vipi, hatukatai tutafanya marekebisho. Tutakaa katika *Cabinet* halafu tutaleta barazani. Sheria hii imepitishwa hapa hapa Mhe. Subeit, huyo Mzanzibari na haki zake. Tumeipitisha sisi wenyewe. Sasa nasisitiza tena lete fikra mimi nitakualika Wizarani pale uje ulete fikra zako tuzifanyie kazi. Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi kuuliza swali dogo la mwisho la nyongeza.
Mhe. Mwenyekiti, katika jimbo langu kuna vijana wengi ambao wameshafikia umri wa kuwa na vitambulisho vya Uzanzibari, lakini sheria iliyowekwa hulazimika kwenda kwa Masheha. La kusikitisha ni kuwa vijana hawa pamoja na kuwa wanakwenda na vyeti vyao *register*, lakini Sheha anavyodai ni kuwa hajapewa fomu serikalini za kuwajazia vijana hao ili waweze kupata vitambulisho.

(a) Mhe. Waziri haoni kuwa kwa vile upande mwengine vitambulisho vinatoka lakini kuna masheha wengine wanafanya hivyo, haoni kuwa masheha wanafanya kwa makusudi, kuona kuwa wananchi hawapati haki yao.

(b) Ukimtizama Sheha ni mtu wa mwisho kiutawala katika serikali hii na hawezi akaamua jambo labda hana pahala pa kuegemea hatuoni kama kuna mpango makusudi katika serikali unaofanywa ili wananchi kukoseshwa haki zao.

(c) Mwisho alisema kuwa kwa wale wenye haki, waliokosa haki zao waende kunakohusika wakapeleke malalamiko hivyo si kumsumbua Mzanzibari kwenda Mahakamani au kokote kunakohusika wakati huu si wajibu wake katika kutetea haki zake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba sana tuziheshimu hizi ngazi za utawala, Sheha ni *govern* katika eneo lake ndio mtawala, ni lazima yeye amfahamu anayeingia na anayetoka na anayeishi. Nakubali wapo baadhi ya masheha kidogo wanayumba. Hilo nakubali kwa sababu tumepata kesi za baadhi ya watu ambao wa Kenya, na watu ambao sio Wazanzibari kwa kudanganya. Wao wamesema ni Wazanzibari kumbe si Wazanzibari, haya yanatokezea.

Lakini ninachosisitiza kwamba tusidharau ile ngazi ya utawala wa sheha, yeye ndiye mtawala, yeye ndiye anapaswa ajue Mwananchi yeyote anayeishi eneo lile. Na yeye hapaswi kumzuia mtu yeyote kumpa barua ya kwenda kuchukua kitambulisho. Kama anafanya hivyo anafanya kwa makosa. Mimi nakuomba kama yupo anafanya Sheha ambaye anafanya hivyo niripotie, tutakaa pamoja tutayarekebisha. Lengo letu kila mtu apate kitambulisho, hilo mtu ni haki yake, hanyimwi mtu. Lakini taratibu tuzifuate Mhe. Salim. Ahsante Mwenyekiti.

Nam. 167

Tatizo la Ajira Zanzibar

Mhe. Saleh Nassor Juma Kny /Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Tatizo la Ajira limekuwa likiongezeka kila mwaka nchini.

(a) Je, kwa nini Serikali inaendelea kutoa ajira za mikataba kwa watumishi waliofikia umri wa kustaafu.

(b) Serikali haioni kuwa kutoa ajira za mikataba kwa wastaafu kunawanyima fursa ya Ajira vijana wengi waliomaliza elimu ya juu ambao wanazagaa bila ya Ajira.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 167 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, kweli tatizo la ajira limekuwa likiongezeka kila mwaka nchini, lakini kama nilivyokwisha kujibu katika swali Nambari 79 (a) jana kwamba serikali imeshaondoa utaratibu wa utoaji ajira za mikataba kwa waajiriwa wa Utumishi wa Umma waliofikia umri wa kustaafu kazi kwa lazima, isipokuwa kwa nafasi ambazo zinahitaji utaalamu, ujuzi na uzoefu maalum na kukosekana mtu mwenye sifa zinazotakiwa kujaza nafasi hiyo.

(b) Nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kwamba kutoa ajira za mikataba kwa wastaafu kunawanyima fursa ya ajira vijana wengi waliomaliza elimu ya juu. Ndio maana katika Sheria ya Utumishi wa Umma Nambari 2 ya mwaka 2011 ajira za mikataba kwa waajiriwa wa Utumishi wa Umma waliofikia umri wa kustaafu kwa lazima zimefutwa, isipokuwa kwa nafasi ambazo zinazingatia sifa maalum ambazo mara nyingi ni adimu kupatikana miongoni mwa vijana wetu. Suala la ajira hizi linalenga kuwafunza na kuwajengea uzoefu vijana wetu katika fani adimu husika.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu ya Mhe. Waziri lakini naomba kupata maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, wanafunzi wetu wanafeli sana maskulini masomo ya sayansi kwa sababu ya kuwepo kwa upungufu mkubwa wa walimu wanaosomesha sayansi, badala yake wanajikita katika masomo ya art ambayo sasa katika Serikali yetu ajira hizi ni chache.

Kwa bahati mbaya kulitokea mtafaruku ya kisiasa, na walimu wengi wakafutwa kazi kule Pemba na wengi wao ni walimu wa sayansi, wanapoomba siku hizi hawapati hizi ajira wanaambiwa kuwa hizi nafasi hakuna.

Je, Mhe. Waziri kwa sababu kasema kuwa wataajiriwa kwa mkataba kutokana na wale wenye umuhimu maalum, ana msimamo gani kwa walimu hao ambao ni walimu wa sayansi hawapati kuajiriwa japokuwa wameshastafishwa kazi kwa manufaa ya kuondoa tatizo la walimu wa sayansi katika visiwa vyetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwanza msimamo wa serikali ni kuwaajiri walimu wa sayansi hata katika mwaka huu wa Bajeti tunaoendelea nao. Idhini iliyotoka ni idhini ya kuwaajiri walimu 500 wa sayansi. Napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba mpaka hivi ninavyozungumza ni kiasi cha walimu 268 tu ndio waliopatikana. Hatukuweza kupata idadi ya walimu 500 wa sayansi.

Taratibu kwa mujibu wa Sheria hii Nam. 2 ya mwaka 2011 kwamba zinapotokea nafasi serikalini kuanzia tarehe 1, Julai baada ya sheria hii kuwa inatumika rasmi, nafasi zinatangazwa. Kila anayehitaji mwenye sifa anatakiwa aombe na aweze kutimiza masharti. Sasa kama kuna walimu ambao walisikia tangazo na wakawa hawakujitokeza mimi sina jibu la kumpa msimamo. Msimamo wa serikali ni kufuatwa sheria iliyopo ya Utumishi wa Umma. Katika kutangaza nafasi hizi tumetoa matangazo na waliohusika waliomba karibu walimu 1350, lakini wenye sifa zilizotakiwa ndio hao ambao nimewasema kwenye jibu la swali la nyongeza.

Nam. 101

Kuongezeka kwa Mimba za Utotoni Pemba

Mhe. Shadya Moh'd Suleiman – Aliuliza:-

Hivi sasa Kisiwani Pemba kuna wimbi kubwa la watoto wa kike wari kupewa mimba. Inaaminika kwamba sababu kubwa ya kuongezeka suala hili ni kutopewa adhabu vijana wa kiume wanaowapa mimba hizo na kupelekea kuwapa mzigo familia ya mtoto wa kike, kwa kulea mimba hiyo pamoja na mtoto baada ya kuzaliwa.

(a) Mhe. Waziri, Wizara yake imefikiria nini kuhusiana na changamoto hii.

(b) Mhe. Waziri huoni kuwa endapo tatizo hili litaendelea kubaki kama lilivyo tutakua na idadi kubwa ya watoto wa mitaani na kuongezeka kwa wimbi la vitendo viovu.

(c) Ili kutatua suala hili, Serikali inachukua hatua gani ya kurekebisha kifungu cha sheria kinachohusiana na suala hili ili upatikane urahisi wa kuwatia hatiani watiaji mimba.

(d) Serikali inachukua hatua gani katika kuwapatia elimu wanafunzi wa skuli ili kupunguza ongezeko hilo.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 101 kama hivi ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi, ni kweli kuna wimbi kubwa la watoto wa kike wari wanaopewa mimba. Mhe. Mjumbe sababu kuu ya wimbi hilo ni kutopewa adhabu kwa wanaume wanaofanya hivyo. Lazima tukubali kwamba ipo haja ya kuchukua hatua madhubuti za pamoja na kuielimisha jamii na hasa sisi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na viongozi wengine wote.

b) Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa hili linaweza kupelekea ongezeko la watoto wa mitaani, hivyo tunahitaji kuchukua hatua za haraka kama nilivyoeleza katika jibu la kipengele A.

c) Mhe. Mwenyekiti, katika kushughulikia hili, Wizara ya Ustawi wa Jamii itawasiliana na Tume ya kurekebisha Sheria hii ili kuweza kupitia na kuainisha Sheria zote zinazokwamisha upatikanaji wa ushahidi ili tuweze kutoa adhabu kali kwa wote wanaohusika na kuwatia watoto ujauzito.

d) Mhe. Mwenyekiti, wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imeandaa mpango wa kutoa elimu kwa wanafunzi wa Skuli kuhusiana na vitendo vya udhalilishaji na kujikinga na mimba za umri mdogo.

Mhe. Shadya Moh'd Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza kunipatia nafasi hii ya kuweza kumueleza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza.

Namuomba Mhe. Waziri atupe takwimu sahihi ya watoto wangapi ambao wanaishi katika mazingira hatarishi katika kipindi cha Juni 2011 mapaka 2012, pamoja na idadi ya watoto waliopewa ujauzito.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa ruhusa yako anistahamilie ili nimletee kwa maandishi jibu hili.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Kwa kweli mimi nakubaliana na swali analoliuliza ya kuwa kuna watoto ambao kuwa wanapewa mimba na kuna uwezekano wa kuongezeka watoto wa mitaani.

Swali langu liko hapa. Siku zote shilingi ina pande mbili, kuna upande una mwenge na upande mwengine kuna picha ya mtu. Kwa kuwa kuna watoto wa kike wanawafuata watoto wa kiume majumbani mwao na wanawalazimimisha kwa nguvu. Je, kuna sheria gani iliyowekwa ya adhabu kwa watoto wa kike wanaofanya vitendo kama hivi ili kuweza kupunguza hayo mazingira hatarishi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kushukuru kwa kunipa fursa hii kuongezea majibu mazuri ya Mhe. Waziri bi Zainab, naomba kwa ruhusa yako nisaidie kumjibu Mhe. Subeit Khamis Faki.

Kwanza anachosema ni kweli huwa inatokea, sheria zetu pia zipo, Sheria ya Jinai Nam. 6 ya Mwaka 2004 ina kifungu kinachosema "Shambulio la Aibu". Kwa hivyo hilo ni kosa kwa mtu ambaye atafanya kitendo kama hicho anaweza kushtakiwa kwa kosa hilo. Lakini pia kuna kifungu kinachosema kama mtu atasaidia kufanya kosa lolote lile la jinai kama la kubaka au kosa la namna yoyote ile, na yeye atashtakiwa kama kwamba yeye mwenyewe kalifanya kosa hilo. Kwa hivyo kwa sheria yetu ya jinai mtu wa namna hiyo anaweza akashtakiwa na akatiwa hatiani kwa makosa kama hayo.

Nam. 28

Matengenezo ya Bandari ya Mkoani

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 71

Kituo cha Afya Pete

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:-

Wananchi wa Pete, kwa muda mrefu wamekuwa hawana Kituo cha Afya na kulazimika kupata usumbufu mkubwa wakufuata huduma za afya katika Kituo cha Unguja Ukuu au Kitogani wakiwemo mama wajawazito na watoto.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kuondoa tatizo hilo kwa kuwajengea kituo chao cha afya?

(b) Kwa kuwa haki ya kupata matibabu ni haki ya kikatiba kwa kila mwananchi, ni sababu gani zinapelekea wananchi wa Pete kutokujengewa kituo hicho tangu Mapinduzi ya mwaka 1964?

(c) Ni lini serikali itachukua hatua ya kuwapatia huduma hiyo wananchi wake kwa kuwajengea kituo cha afya hatua ambayo itanisaidia Mwakilishi wao kupata usingizi?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Baraza lako tukufu swali lake Nam. 71 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti Sera ya Afya imezingatia kutoa fursa sawa ya upatikanaji wa huduma za afya za msingi za tiba na kinga zilizobora kwa wote ikiwa pamoja na huduma ya afya ya uzazi na mtoto, uchunguzi mapema, urekebishaji, magonjwa ya muda mrefu na dharura kwa kujumuisha uratibu wa rufaa wenye ufanisi. Katika kufanikisha hayo vigezo mbali mbali vimetumika ikiwemo masafa baina ya kituo hadi kituo, ambayo ni kilomita tano za mraba.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjuilisha Mhe. Mwakilishi kwamba, kwa sasa serikali kupitia Wizara ya Afya haina mpango wa kujenga vituo vyengine vipya. Utafiti uliofanywa kwa kutumia mfumo wa kutoa taarifa kimaeneo (*Geographic Information System*), unaonesha kwamba Zanzibar imefikia asilimia 99 na iliyobaki ni 1 ambayo ni bahari.

Kwa kweli asilimia kubwa ya vituo vyetu vya afya na maeneo yanayopendekezwa kujengwa vituo vipya yako chini ya kilomita tano, mfano halisi ni Pete Kitogani na Pete Unguja Ukuu, ambavyo vyote hivyo masafa yake hayazidi kilomita tatu.

Kipaumbele cha wizara kwa sasa ni kuimarisha vituo vilivyopo kwa kuongeza wafanyakazi wenye sifa, vitendeakazi vyenye ubora pamoja na ukarabati wa vituo na ujenzi wa nyumba za wafanyakazi. Pamoja na huduma zinazotolewa kwenye vituo hivyo, pia kuna huduma za mkoba (*Outreach Services*), ambapo Mhe. Mwakilishi kwa kushirikiana na Kamati za Afya za Vijiji zinaweza

kushauriana na Wakuu wa Vituo juu ya aina ya huduma wanazopenda zitolewe kwa njia ya mkoba.

Nam. 171

Mafunzo kwa Vyama vya Ushirika

Mhe. Salma Mussa Bilali – Aliuliza:-

Jumuia ya Vyama vya Ushirika Tanzania, Chuo cha Ushirika Moshi kilikuwa na matawi yake wawili hapa Zanzibar (moja Unguja na jengine Pemba). Matawi hay yalitumika kwa ajili ya kutoa mafunzo ya ushirika kwa watendaji, viongozi na wanaushirika mbali mbali. Kwa hivi sasa matawi hayo yamefungwa. Tulio wengi hatujui ni kwa sababu gani. Ukweli usiofichuka ni kwamba, Zanzibar bado elimu ya ushirika inahitajika sana.

(a) Je, taaluma ya ushirika kwa makundi niliyoyataja hapo awali inapatikanaje?

(b) Je, Mhe. Waziri huoni umuhimu wa kuwa na pahali mahsusi pa kuendeshea mafunzo haya au kuchukua hatua za kuishauri taasisi hiyo ya Ushirika ya Tanzania Bara kuja kuanzisha tena matawi yake kwa kushirikiana na serikali au taasisi nyengine yoyote?

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 171 kama ifuatavyo:-

(a) Nakubali kwamba elimu ya ushirika Zanzibar bado inahitajika sana kwa watendaji, viongozi na wanaushirika wote kwa ujumla. Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu imeliona hilo baada ya kufungwa matawi ya Chuo cha Ushirika hapa Zanzibar, ikiwa cha upatikanaji wa elimu ya ushirika kimeathirika sana. Wizara kupitia Idara ya Ushirika imebeba jukumu zito la kutoa taaluma hiyo.

Aidha wizara, ili kuunga mkono utoaji wa taaluma hiyo kwenye vyama imeanzisha mashirikiano ya karibu na taasisi nyengine mbali mbali kama vile Benki ya *CRDB*, *Program* ya *AASP*, *PADEP* na Shirika la *Action Aid* na kadhalika.

Pia ili kujenga ushindani kwenye vyama wizara imekuwa ikishirikiana na wataalamu mbali mbali kutoka Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi pamoja na mashirika mengine ya ndani na nje, ili kupata mahitaji halisi ya mafunzo. Pamoja na hatua zote hizo wizara yangu inakiri kwamba bado taaluma ya ushirika inahitajika zaidi na kuna haja ya kuongeza juhudi hasa wakati huu wa kuimarisha Vyama vya Ushirika hapa Zanzibar.

(b) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu inafahamu kwamba upo umuhimu wa kuwa na mahala mahsusi pa kuendesha Mafunzo ya Ushirika hapa Zanzibar. Kwa hivyo, uongozi wa wizara yangu umeshaanza mazungumzo juu ya suala la Uongozi wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, ili kuona jinsi ya kuwepo matawi ya Chuo cha Ushirika na *Study* za Biashara hapa Zanzibar. Lakini lengo tuwe na taasisi yetu wenyewe hapa Zanzibar, ambayo itakuwa inatoa mafunzo ya Vyama vya Ushirika. *(Makofi)*

Mhe. Salma Mussa Bilali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri. Kwa kweli kumekuwa na wimbi kubwa la kusajili Vyama vya Ushirika ambavyo vinakuwa si endelevu, inawezekana ni kutokana na ukosefu wa hii elimu ama mitaji ya kujiendesha.

Je, wizara yako imejipanga vipi katika kufanya juhudi za makusudi, ili kuvipatia mitaji vyama hivyo kwa ajili ya kuwa endelevu na waweze kujiajiri na kujipatia kipato wanachama hao?

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, kwenye jibu langu mama nimesema tumekiri kwamba kuna tatizo la taaluma ya elimu ya Vyama vya Ushirika na hivi sasa jukumu hilo limebebwa na Idara yangu ya Ushirika kwa kushirikana na Benki ya *CRDB* kupitia taasisi kama vile *AASP* na *Action Aid*.

Vile vile tumesema kwamba tutashirikiana na wenzetu wa Chuo Kikuu cha Ushirika kule Moshi, lakini hatimaye Zanzibar tuwe na taasisi kama hiyo ambayo itakuwa inajitegema wenyewe.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kuweza kunipa nafasi ya kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri lenye vifungu (a) na (b).

(a) Mhe. Waziri, ametueleza hapa kwamba kuna mpango wa kuwa na chuo chetu wenyewe hapa Zanzibar. Je, Mhe. Waziri katika bajeti

yako ya mara hii mpango huo umo na tayari umeshatenga fedha hizo?

(b) Mhe. Waziri, pamoja na kuwa umejitahidi sana kuwafundisha hawa wanavikundi na kuwashajihisha kuomba fedha za mafunzo kwa kupitia mabenki. Je, huoni iko haja sasa hawa wenye mabenki ukawaomba, ili riba ikawa ndogo kwa wanavikundi kwa ajili ya kupata maendeleo? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, kwanza sikusema kama nitaanzisha taasisi hiyo, isipokuwa nimesema kwamba wizara ina lengo, kwa sababu siwezi kuweka kwenye bajeti kama kitu ambacho hakipo, kwani hivi sasa hakipo ndio maana yake hatukuingiza kwenye bajeti. Lakini lengo tunalo kama si mwakani basi mwaka ujao. Kwa hivyo, hivi sasa tutaendelea kutumia uzoefu wa Chuo Kikuu cha Ushirika kule Moshi.

Pili ni kweli kwamba taasisi zetu, Vyama vya Ushirika pamoja na wananchi binafsi suala la riba limekuwa likiwapa matatizo makubwa Mhe. Mwenyekiti. Kwa maana hiyo, tumeanzisha utaratibu maalum pale wizara sisi kutokana na bajeti ambayo itaanza mwaka huu tukijaali, kwamba tujaribu kwa kadri itakavyowezekana kwanza kuzungumza na mabenki kupunguza riba hizo. Vile vile mikopo ambayo itasimamiwa na wizara yetu moja kwa moja tunakusudia kuondosha riba hizo na kutumia utaratibu wa Benki za Kiislamu. *(Makofi)*

Nam 75

Huduma ya Umeme Makunduchi

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny: Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:-

Hospitali ya Makundichi ni moja kati ya hospitali inayotegemewa na wananchi wengi katika Mkoa wa Kusini, lakini ni muda mrefu inakabiliwa na tatizo la kukosekana kwa huduma ya umeme wa uhakika.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kuwaondolea tatizo hilo?

(b) Kwa kuwa hospitali hiyo ipo katika mpango wa kuanzisha Kitengo cha Mifupa, huduma hizo zitaweza vipi kufanyika kama huduma za umeme zimekuwa sio za uhakika na kuathiri huduma za picha (*X-Ray*) na Benki ya Kuhifadhi Damu katika hopitali hiyo?

(c) Je, ni tatizo gani linalopelekea huduma ya umeme kutokuwa ya uhakika katika hospitali hiyo wakati miundombinu yote ya umeme ipo katika hospitali ya Makundichi, lakini umeme umekuwa ukikatika kila mara na wakati mwengine kuwa mdogo kama kibatari?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, ahsante naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 75 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, tatizo hili tayari limeshapatiwa ufumbuzi.

(b) Mhe. Mwenyekiti, huduma za umeme kwa sasa ni za uhakika katika hospitali hiyo baada ya matengenezo hayo. Pia shirika tayari limeshafanya matayarisho ya kufungua Kituo Kidogo hapo Makunduchi kwa upande wa Mkoa wa Kusini, ambacho kitakuwa na mafundi kwa muda wote, kwa ajili ya kufanya matengenezo ya mkoa huo.

(c) Mhe. Mwenyekiti, tatizo hilo limeshapatiwa ufumbuzi kwa kufanyiwa matengenezo ya fuse ambazo zilikuwa zikiungua mara kwa mara na kulazimisha mafundi kutoka mjini kwenda kuishughulikia line hiyo, ambayo ilikuwa na matatizo makubwa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri.

Kwa kuwa Hospitali ya Makunduchi iko katika Kijiji cha Makunduchi, ambacho ni kijiji cha historia sana katika nchi hii. Vile vile Makunduchi wanatoka watu muhimu na mashuhuri sana akina marehemu Sheikh Ameir Tajo, Marehemu Rais wa Zanzibar wa Awamu Nne Sheikh Idrisa Abdulwakili, Spika wetu wa Baraza la Wawakilishi, Jaki Mkuu wa mwanzo wa Zanzibar Mhe. Sheikh Ali Haji Pandu, Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, Naibu Katibu Mkuu wa CUF Mhe. Ismail Jussa Ladhu. *(Makofi)*

Je, kuendelea kuchelewasha huduma ya umeme pale hospitali si kuwadhalilisha viongozi wetu hawa? *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu ikilitambua hilo kwamba Viongozi Wakuu wengi

wa serikali wanatoka katika Kijiji cha Makunduchi, basi ndio maana ikaharakisha kwa hali zote na kufanya jitihada iwezekanavyo, ili kuliondoa tatizo hili. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa tatizo hilo limeondolewa na jitihada za kurekebisha matatizo mengine zinaendelea kurekebishwa. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kuweza kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri lenye vifungu (a) na (b).

(a) Hivi ni sababu zipi ambazo wizara yako za kutokutoa kipaumbele katika Vituo vya Afya, ili kuwapa umeme wa uhakika?

(b) Utakubaliana na mimi kuwa mpaka hivi sasa kwamba Kituo cha Afya cha Kitope kimekatwa umeme?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu inaipata vipaumbele sana Vituo vya Afya kwa ajili ya kurekebisha matatizo ya umeme. Kwa mfano, katika hicho Kijiji cha Makunduchi ambacho nimekielezea mwanzo.

Kuhusu suala la Kituo cha Afya cha Kitope kukatiwa umeme kwa kweli taarifa hiyo sina. Lakini kama lipo hilo Mhe. Mwakilishi nakuomba tushirikiane na twende pamoja na baadaye nitalisimamia mwenyewe na umeme tutaurejesha mara moja. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwanza katika ile orodha aliyoita Mhe. Saleh Nassor Juma (Muasisi) naomba nimuongezee katika Baraza hili ni pamoja na watu wanaotoka Makunduchi pia na Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdillah Jihadi Hassan. Lakini kuliko wote muhimu Mnadhimu wa CCM katika Baraza hili Mhe. Salmin Awadh Salmin. *(Vicheko/Makofi)*

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba niulize swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, wakati Hospitali ya Makunduchi ambayo ilijengwa na Hospitali nyengine tatu zikiitwa *Cottage Hospitals*, ilipokuwa inajengwa ilipatiwa pia miundombinu ya umeme wa jua na wakati ule ukitembelea maeneo haya zilikuwa zinafanyakazi vizuri.

Sasa naomba kusaidiwa kwamba katika kipindi hichi nini kimefanyika hata miundombinu hiyo, iliyokuwa imewekwa ya kutumia umeme wa jua ikawa imeathirika hata leo tunazungumzia matatizo ya umeme wetu huu wa kawaida?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na suala la umeme wa jua ambao umewekwa katika hospitali hiyo naomba nikae na Mhe. Waziri wa Afya, ili nimuulizie hatua gani pengine iliyofikia au kuna sababu gani zilizosababisha kuondolewa kwa umeme huo. Lakini kwa umeme wa Shirika la Umeme basi huo kwa hivi sasa uko salama, tena uko vizuri na matatizo yote tumeshayaondoa. *(Makofi)*

Nam. 119

Uboreshaji wa Timu ya Taifa Zanzibar

Mhe. Abdi Mosi Kombo – Aliuliza:-

Wakati wa Serikali ya Awamu ya Kwanza ya Marehemu Mzee Abeid Amani Karume zilikuwa zikialikwa timu mbali mbali za nchi za nje, kwa ajili ya kuipima nguvu Timu ya Taifa ya Zanzibar, kama vile nchi za China, Ujerumani, Congo na Sudan.

Je, serikali kupitia Wizara hii ya Habari ina mkakati gani wa kurekebisha mpango huo, ili kuwajenga vizuri vijana wetu wanao liwakilisha taifa na kufanya wananchi wa Zanzibar wanaopenda michezo waingie hamu ya kupenda michezo ya kwao?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 116 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Baraza la Michezo lina mpango wa kurejesha utaratibu uliokuwepo katika Serikali ya Awamu ya Kwanza ya Mheshimiwa Marehemu Mzee Abeid Amani Karume kwa kualika timu kutoka nje kwa ajili ya kuipa uzoefu na nguvu Timu ya Taifa ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mpango huo serikali inaendeleza utaratibu wa sasa wa kuipeleka Timu hiyo ya Taifa nchini Misri. Kwa kweli kila mwaka kupiga kambi, kujiandaa kwa Mashindano makubwa ya *Challenge*.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsnate sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hivi karibuni Mhe. Waziri alitangaza kuwapatia zawadi Timu ya Taifa ya Zanzibar (*Zanzibar Heroes*), pindipo itapata ushindi katika Mashindano ya *Challenge*. Lakini kutokana na hali ya mabadiliko ya sasa kwamba zawadi ya vespa imepitwa na wakati.

Je, haoni kwamba itakapochukua ubingwa wa *Challenge* Timu ya Taifa Zanzibar (*Zanzibar Heroes*) kwamba kuna haja ya kuwazawadia gari kuliko vespa? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mhe. Waziri alisema kuwa siku timu yetu ilipokuwa inaondoka aliwaahidi kama watapata ushindi wa mwanzo basi atawazawadia kila mtu shilingi milioni 1,000,000/=.

Lakini walipata ushindi wa tatu na kuwazawadia kila mtu shilingi 250,000/= na Makocha ni shilingi 150,000/=. Hiyo Mhe. Mwakilishi ni faraja pekee kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kufanya hivyo.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyonge lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Takriban skuli zote za Unguja na Pemba kulikuwa na michezo kama vile ngojera, riyadha, kwaya na kadhalika. Je, ni sababu zipi zilizofanya kuondoshwa kwa michezo hiyo maskulini?

(b) Je, Mhe. Naibu Waziri huoni kuwepo kwa michezo hiyo ni kuwaongezea vipaji watoto wetu na kupata wachezaji bora na kuongezea uwezo Timu yetu ya Taifa?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli na sisi pia tumepitia humu, lakini kwa sababu ya usumbufu uliokuwa ukitokea maskulini. Kwa kweli hivi sasa tayari tumeshakaa na Wizara ya Elimu, ili kuwa na Mpango Mkakati wa kurejesha michezo maskulini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, swali lake la kifungu cha (b) naomba alirudie sikulisikia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, rudia swali lako kifungu cha (b).

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, huoni kuwepo kwa michezo maskulini kuwaongezea vipaji watoto wetu, kwa ajili ya kuiongezea uwezo Timu yetu ya Taifa?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli suala hilo ni muhimu kwa sababu michezo ni afya,

michezo maskulini na hata kama si maskulini basi michezo ni ajira. Vile vile michezo inaingiza kipato kwenye nchi yetu hii ya Zanzibar. Kwa kweli kitu hicho ni kizuri na kama nilivyo swali lako la kifungu (a), basi tutafuatilia zaidi kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa ajili ya kuirejesha michezo hii maskulini. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa Timu yetu ya Taifa inahitaji wachezaji wazuri na wenye kipaji tena wenye uwezo mkubwa.

Vile vile katika Baraza hili Mhe. Waziri alituahidi kama wataanzisha michezo katika wilaya, majimbo pamoja na mikoa, kwa ajili ya kupata wachezaji wazuri wenye vipaji kwa lengo la kuongeza nguvu katika Timu yetu ya Taifa. Je, hivi Mhe. Waziri azma hiyo imekuwa au bado ipo na kama ipo ni lini hasa kupitia wizara hii itaanzisha michezo katika wilaya na majimbo yetu, ili kupata watu wenye vipaji kwa lengo la kuongeza uwezo katika Timu yetu ya Taifa? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ni Mhe. Mwakilishi wangu wa jimbo basi wewe mwenyewe binafsi hushirikiani na mimi kuhusu masuala ya michezo. Sasa nakuomba tushirikiane, ili michezo mawilayani tuendeleze pamoja na mikoani. Kwa kweli Mhe. Mwakilishi nakuomba uwe karibu na mimi nikiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo tena ni mpiga kura wako wa Jimbo la Micheweni. *(Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri lakini nilimuomba na wala sio jimbo langu tu, nilimuomba kuhusu mikoa, wilaya pamoja na majimbo, ili kuibua wachezaji wazuri wenye vipaji kwa ajili ya kuisaidia Timu yetu ya Taifa. Kwa upande wa jimbo langu niko tayari kushirikana na yeye, je wilaya na mikoa nitashirikiana na nani? *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kufafanua zaidi swali la Mhe. Mwakilishi. Lakini kabla ya hapo naomba nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kujibu ufasaha majibu ya Mhe. Mwakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, michezo iko katika wilaya zote na ninamuomba sana Mhe. Mwakilishi arudi Wilaya ya Micheweni akashirikiane na *ZFA* ya Wilaya ya Micheweni na akaangalie namna gani mashindano haya yanaendeshwa. *(Makofi)*

Vile vile kama ni Mwakilishi wa Jimbo basi ningemuomba pia aige mifano ya Wawakilishi wengine ambao tayari wameshaanzisha Ligi za Majimbo katika majimbo yao. Kwa mfano, hata Mhe. Mwenyekiti wewe mwenyewe naomba nikupongeze kwa hili na Wawakilishi wengine ambao wameanzisha hili. Kwa kweli hili ni jambo letu sote naomba tushirikiane, lakini zaidi arudi katika wilaya yake aone namna gani *ZFA* Wilaya ya Micheweni ilivyojidhatiti katika suala hili. *(Makofi).*

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Fedha na Usimamizi wa Mapato 2012

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea. Kwa hivyo, tumuombe Mhe. Saleh Nassor Juma anazo dakika zake 10, lakini kila akizipunguza itakuwa ni vizuri zaidi kwa sababu leo ni siku ya Ijumaa. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kumalizia hizi dakika zangu 10. Lakini kabla sijaanza naomba niendelee kuipongeza SMZ, kama kuna mwaka ambao serikali yetu hii Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Umoja wa Kitaifa, basi kama kuna mwaka iliyopata Mhe. Waziri makini, mahiri na mwenye maneno na matendo basi ni mwaka huu. Kwa kweli ni mtaalamu sana katika kupanga na kuyasema maneno kwa hilo nampongeza sana. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa nadhani niende moja kwa moja kwenye suala zima na nilikuwa nimeacha kwenye ule utozaji wa shilingi 1,000/= kwa wasafiri wanaotoka Pemba kwenda Unguja au wanaotoka Unguja kwenda Pemba.

Kwa kweli mimi nasema Mhe. Mwenyekiti, hebu serikali iangalie upya suala hili, kwa kadri ninavyomfahamu Mhe. Waziri najua anacho kichwa kilichoelimishwa na moyo unaoshaurika, anao wataalamu wanaongozwa na ndugu yangu Khamis Mussa ambao ni makini katika maneno na mahiri sana katika matendo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naamini hii kodi ya shilingi 1,000/= kwa wapemba wanaokuja Unguja na Watumbatu wanaokwenda Pemba, basi naamini kwa kutumia busara zao wataiondosha, kwa sababu mimi sioni *logic* na mimi ni mwanasiasa na sio mtaalamu, taaluma yangu mimi ni katika viumbe akiwemo binadamu, hivyo katika mambo ya uchumi si mtaalamu.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali itizame vizuri katika hili hakuna *logic*, kwa sababu Wapemba wanapokuja Unguja wanalipa ada ya bandari pale na tiketi tayari wameshakata, boti wanazosafiria ni za watu binafsi akina Bakharesa ndio wanaosafiria boti zao na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haina meli hata moja. Sasa wanataka nini tena pale kutukatia shilingi 1,000/= na wao hawana meli, hivi 'wanawa uso kwa mikungwa' na hili ni tatizo. *(Makofi)*

Sasa mimi nawaambia SMZ sisi Wapemba tunasema kwamba 'musinawe uso kwa mikungwa'. Kwa maana hiyo, ni vyema kuwapa nafuu. Hivyo, ni vigezo gani walitumia SMZ hata wakatuletea kodi hii kama ni masafa basi tujue, kwa sababu ikiwa wame-*regard* masafa basi kutoka kwa Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein Mkanyageni na kwa Mhe. Haji Faki Shaali kule mpaka kufikia mnarani ni masafa makubwa zaidi ukilinganisha na Mkoani na Nungwi kama ni masafa haya mmefanya kosa, basi na wale wanaotoka Mkanyageni kwenda Konde na wao muwakatishe kwa sababu ni pakubwa zaidi. Ikiwa ni bahari nina wasi wasi basi na wale Watumbatu nao wakija Mkokotoni muwatoze shilingi elfu. Mmetumia *logic* gani, sioni *logic* mimi iliyotumika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani hili jopo la wataalamu linaloongozwa na Mhe. Khamis Mussa pamoja na mwanangu pale Waziri wa Fedha na Uchumi wakatumia busara zao naamini wana vichwa vilivyoelimishwa mno, wana mioyo inayoshaurika nawashauri katika hili waondoshe kabisa shilingi elfu moja kusudi Wapemba na ndugu zangu Watumbatu wawe wanapita kama kawaida bila ya kutozwa. Mhe. Mwenyekiti, hilo ni moja.

Pili, nilisema kwamba tuwe makini katika kusimamia mapato vyanzo vipo, ukiacha mbali na hivyo vilivyokaliwa na hilo jinamizi la Muungano, vipo vyanzo hatuzisimamii vizuri vya humu humu. Kwa mfano, hivi sasa kuna shilingi 500 zinazotozwa kwa gari zinazoingia *airport*, sasa hazisimamiwi vizuri. Mimi juzi nilikuwa na mgonjwa anakwenda Dar es Salaam kapewa *refer* kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja hiyo nauli tumechangishana nauli ya ndege, tunachangishana nauli kufika pale katozwa shilingi 500, kapita Katibu wa wizara fulani namuona kwa jicho langu hata shilingi hakutoleshwa pale wakati yeye pesa anazo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini hawa Makatibu, Wakurugenzi magari ya serikali yasilipishwe tulipishwe sisi tu, ni maonevu makubwa. Mimi nadhani serikali isiwe *bias*, hakikisheni gari yoyote pale inayoingia iwe inalipa kwa sababu hatuwatendei haki wananchi wetu. Kwa kuwa wengine nauli wanachangiwa halafu watoe tena shilingi 500 ni tatizo kubwa sana wakati hawa Maafisa Wadhamini, Makatibu Wakuu wanazo pesa wagonjwa wanakwenda kwa matatizo na wanalipa kwa nini hawa wakubwa wasilipe? Basi tuvisimamieni vitu kama hivi.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani nimalizie kwa kutoa tanbihi, nitoe tanbihi kwa Wazanzibari. Mama Asha Bakari Makame juzi alisema kwamba amani hakuna pahala ambapo unaweza kuinunua, amani ikishapotea haipatikani tena, hakuna *super market* inayopatikana amani kabisa kabisa. Sasa Mhe. Mwenyekiti nawashauri Wazanzibari wenzangu wakiwemo UAMSHO mimi si UAMSHO lakini Muungano siutaki. Mimi si UAMSHO lakini naukataa Muungano kuliko wao UAMSHO, sasa pahala pekee ninaposubiri mimi ni kwenye Tume ya Maoni, tushikamane Wazanzibari tuwe kitu kimoja japo msiwe na mawazo niliyonayo mimi ya kukataa Muungano kila mtu ana mawazo yake. Lakini mimi naukataa Muungano kabisa siutaki lakini sifanyi fujo, nimetulia nasubiri Jaji Warioba aje na kamati yake hapa nifanye vitu vyangu.

Kwa hivyo, nawaomba ndugu zangu UAMSHO, ndugu zangu Wazanzibari tushikamane tuwe kitu kimoja tuache tofauti zetu za kisiasa, tuache tofauti za kidini tuwe kitu kimoja tuhakikishe kwamba tunajinasua katika jinamizi hili la Muungano ambalo limetunamia katika misingi ya kisiasa na kiuchumi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naiunga mkono hoja ya mwanangu Mhe. Waziri, Omar Yussuf Mzee ahsante sana.

Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Asiye na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, mimi najua kwamba leo ni Ijumaa na tuna majukumu mengi lakini naomba nitumie muda mfupi sana kufafanua jambo dogo ambalo wananchi wanaweza pengine wasilielewe vibaya huko nje.

Mhe. Mwenyekiti, jana wakati Mjumbe mmoja anachangia hii zaidi alikuwa ananizungumza mimi binafsi, sasa mimi sitaki nimzungumze yeye. Lakini nataka niseme kwamba serikali kwa maana ya Mawaziri, Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi sote humu tunawajibika kwa pamoja ndani ya Baraza la Wawakilishi. Sasa hawezi Waziri mmoja au Mjumbe mmoja wa Baraza la Mapinduzi akaja hapa akapingana na Mswada wa serikali ambao umetoka ndani ya Baraza la Mapinduzi. Kwa hivyo naomba kwanza hilo lieleweke kwa sababu wananchi wamepotoshwa na hawakupotoshwa humu tu, lakini baada ya hapa tena kuna mwengine alikwenda kupotosha mpaka nje.

Mhe. Mwenyekiti, naomba wananchi wafahamu kuwa kwa mujibu wa kifungu cha 43 (5) cha Katiba ya Zanzibar, serikali inawajibika kwa pamoja ndani ya Baraza la Wawakilishi, hawezi Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Mhe. Said Ali Mbarouk akaja hapa akalikataa suala la Wizara ya Elimu au siwezi mimi Mhe. Haji Faki Shaali Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi na serikali hii inaongozwa na Baraza hilo lenye wajumbe 23 na mimi nikiwa nimo nikaja nikalikataa suala lile.

Kwa hivyo, naomba hilo wananchi kwanza walifahamu na kama wamepotoshwa wafahamu kuwa hiyo ndio Katiba, sisi hapa tukiongozwa na Makamu wa Pili wa Rais tunawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi. Kwa maana hiyo mimi nitakuwa siheshimu kiapo changu nilichokula wala siheshimu chama changu kilichonipeleka serikalini kama nitakwenda kinyume na matakwa ya katiba yangu, hilo la kwanza.

Lakini la pili sasa Mhe. Mwenyekiti nije katika hiyo hoja yangu niliyozungumza juzi, nafikiri *Hansard* iko vizuri. Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mwalimu na nina huruma sana na watoto, nilichokizungumza juzi kwamba hii ada ya shilingi 1,000 inaumiza, lakini ni nani wa kuwaonea huruma kati ya wazee na watoto? Sasa kama mimi mwalimu na Maalim Saleh nafikiri vile vile ataniunga mkono maana yeye alikuwa mwalimu na hata wasiokuwa walimu sote ni wazazi. Mimi nikasema kwamba jamani inaumiza lakini watoto wetu wanaumiza zaidi na jamii yoyote inazingatia watoto, hata katika vita na maafa wa kuhurumiwa ni watoto. Kwa hivyo, mimi nikaomba sana kwamba pamoja na kuwa wazee wataumia kutoa shilingi 1,000 kwa safari, lakini hii haitumiki kwa anasa wala maposho na mambo mengine hizi zinakwenda kununuliwa madawati. Sasa je, kuna ubaya gani sisi wazee kutoa shilingi 1,000 wakanunuliwa watoto wetu madawati? Hilo nadhani ndilo nililolizungumza wala sikwenda zaidi ya hilo.

Mhe. Mwenyekiti, ilibidi nilisema hilo ili kwamba ule upotoshwaji uliofanywa wananchi wafahamu. Kwa sababu ungeishia humu ndani ya Baraza wala nisingesimama hapa, lakini bahati mbaya ule upotoshwaji ulikwenda kufanywa mpaka nje, sitaki kutaja watu majina mimi ni mtu mzima sio *simple mind* lakini nilisema nisimame niseme hayo.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba hakuna Muislamu zaidi atakayekuja akamshinda Mtume Muhammad *(S.A.W)*, vyovyote utakavyosema wewe Muislamu basi hutamshinda Mtume Muhammad (*S.A.W*) Uisilamu wako. Na wala hatokuja Mkatoliki kwa sasa hivi akamshinda Benedict wa sita sijui au kumi na sita kwa Ukatoliki wake. Na mimi niseme hivi, Mwakilishi yoyote ambaye atasema anaipenda nchi hii basi hatanishinda.

Tena nataka niongeze zaidi Mhe. Mwenyekiti, kama kuna Mwakilishi yoyote Mkoa wa Kusini Pemba ambaye jimbo lake limebadilika na *challenge* hakuna kama Jimbo la Mkanyageni. Kwa hivyo nilitaka niseme hilo ili isijeikaonekana kwamba wengine wanapenda wananchi, wengine hatupendi, wengine wanapenda maendeleo na wengine hatupendi maendeleo.

Mhe Mwenyekiti, nakushukuru sana ahsante.

Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitangulie kukushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia na mimi hoja ya Mswada huu wa Fedha. Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani na mambo mawili matatu tu ya kuchangia, kwa sababu huu mswada bahati nzuri umechangiwa na Waheshimiwa wengi, lakini bahati mbaya sana hawakuwa wakichangia mswada nasikitika kusema hivyo, lakini walichangia zaidi kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa kwamba labda maudhui ya mswada lakini sio hasa vifungu vya mswada. Kwa sababu vifungu vya mswada nadhani vyote vilivyowasilishwa hakuna vifungu ambavyo vilihojiwa. Labda na mimi niombe tu kwamba labda nifafanue mambo mawili matatu mengine katika hayo maudhui.

Suala la kwanza lilikuwa ni lile suala la kwamba pengine mswada huu usingehitajika au tusingehitaji kurekebisha kodi kama tungeweza kudai yale madai lukuki. Sijui kama kuna idadi kubwa zaidi ya lukuki basi hiyo ni lukuki wa lukuki aliyosema Mhe. Jussa, alisema kama tungeweza kudai hayo basi isingekuwa na haja ya kuleta mswada huu. Na mimi nikubaliane naye, lakini nikubaliane naye kusema kwamba, kama tungezipata hizo basi pengine isingekuwa na haja, lakini kawaida ya pesa tungezipata pengine tungekuwa tumeshazitumia, tumeshazimaliza na tungehitaji hizi ambazo tunaziomba humu ndio kawaida ya pesa ilivyo na tungekuwa na mambo mengi tu ya kuzifanyia kwa sababu mambo ya kuzifanyia yapo. Hizi pesa ni nyingi lakini na mambo ya kufanya kwa nchi hii yapo na ndio maana Mhe. Mwenyekiti, tunasaidiwa, tukumbuke kwamba mambo mengi ya nchi hii tunasaidiwa sasa hivi, lakini tungekuwa na pesa zetu tungefanya wenyewe.

Tumesaidiwa *wire* tu wa kutoa umeme kuleta hapa, wa kupeleka umeme Pemba tumesaidiwa, mabarabara tunasaidiwa, bandari tunasaidiwa, afya tunasaidiwa, elimu tumejengewa skuli mpaka kwetu kule skuli ya kisasa kabisa na barabara ya kisasa inajengwa sasa hivi, lakini tumesaidiwa. Sasa shida ya pesa tunayo lakini na kutumia tunazo sehemu nyingi tungezipata tungezitumia na zisingetosha kwa hayo mambo yetu, bado tungehitaji kukusanya kodi zaidi. Mimi naomba hilo tulifahamu sana tusiwape watu *impression* ya kwamba tungepata pesa hizi basi tusingekuwa na haja ya

kuhitaji kupandisha kodi, tungetumia na shida zetu bado zipo za kutumia na bado haja ya kupata pesa zaidi ingekuwepo.

Kwa hivyo, niseme Waheshimiwa sisi ni viongozi ni vizuri tuwaelekeze, kuongoza njia ni kuelekeza sasa ni vizuri tuwaongoze wenzetu vizuri tusiwape matumaini ambayo pengine wala wasingejua. Kwa sababu hata hao Bara ambao tunawadai hivi wamefika wapi, si wanasaidiwa kila siku? Wanasaidiwa kuliko sisi, pamoja na kula na hizo za kwetu tunazowadai, lakini bado umasikini wao haujaondoka upo, bajeti yao wanavyosaidiwa ni kubwa zaidi kuliko tunavyosaidiwa sisi. Hili mimi nadhani ni vizuri kama viongozi tukaliweka vizuri likafahamika.

Lakini vile vile hili la kudai pengine pia nasema tukubali kwamba sote Baraza hili pamoja na serikali sisi mmetutuma nikama madereva mmetupa tuendeshe, kesho mnaweza mkasema jamani kaeni pembeni tutafute dereva mwengine. Maana Baraza hili ni Wawakilishi wananchi na katiba yetu imesema mamlaka yote yanatoka kwa wananchi.

Lakini sasa ukishakuchagua dereva ambaye umemuamini, kwa sababu katika kitu ambacho ni kizuri katika serikali ya sasa hivi hatuna tatizo la *legitimacy*, maana serikali hii inaongozwa kwa ridhaa ya 100% ya Wazanzibari, ukichanganya kura za rais na za Makamo wake wa Kwanza maana yake tuna ridhaa ya 100% ya Wazanzibari na hawa wote wamo kwenye serikali hii ndio wanaoendesha, sasa mkianza watu kuwaambia kwamba bwana hawa madereva mlowapa ni wasi wasi mnaanza kuwatia mashaka abiria, ukiwatia mashaka abiria dereva atakosa kazi lakini na wewe mwenye gari utakosa biashara. Nadhani tunafahamiana, abiria ukiwatia wasiwasi wewe mwenye gari utakosa biashara dereva atakachokosa ni kazi, kazi atatafuta nyengine lakini biashara kutafuta nyengine shida.

Sasa mimi nadhani tukubaliane kwamba juhudi tunaifanya ya kudai wengine tumelelewa kwenye maadili ya kuheshimu wakubwa, kuheshimu watu, lakini katika kudai haya tunafika pahala mpaka unaonekana huna nidhamu, yote ni katika kudai. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini nadhani sote tukubali kwamba wako watu wanaitwa wadaiwa sugu na hawa wako kila pahala na kwenye biashara ndio maana wana principle ya Uhasibu wanaita *bad debts*, *bad debts principle* hiyo ingekujaje kama hakuna wadaiwa sugu, mtu unamdai mmekubaliana vizuri, mikataba ipo, lakini inafika pahala hakulipi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi wanambie humu ndani hamna watu wanaodai watu tena pengine Waheshimiwa wenzao na wamewafanyia tabu kuwalipa, hivi

wamepigana nao? Lakini humu humu ndani tumo tunaodaiwa tunafikishwa kutaka kupelekwa Mahakamani hatulipi na Waheshimiwa haina haja ya kutajana. Sasa hii ni hulka ni tabia lakini huwezi kumlaumu anayedai tizama juhudi yake tunajitahidi Mheshimiwa. Mimi naomba kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kwamba tunajitahidi kudai kwa nguvu na uwezo lakini kama kuna mtu anaona anaweza akatusaidia kudai liko Bunge akatusaidie kudai, lakini na kwenye vikao tunaweza tukamualika tukamsikia yeye atasema lipi kubwa ambalo sisi hatujalisema katika kudai.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hii ni *reflection*? Kweli ni miongoni mwa matatizo ya Muungano wetu. Tumesema, mimi nimewahi kusema na naomba nirudie kwamba kweli katika Muungano wetu kuna maswali ambayo hayana majibu na bado hayana majibu. Kwa sababu ukiniuliza mimi na mimi nimetoa *challenge* kwa sababu nimesema hivyo tangu mwaka 2005 hakuna mtu aliyenipa majibu mpaka leo. Sasa hii fursa ambayo imetokea basi madhumuni yake ndio hayo yatatusaidia kusawazisha yale ambayo yana kasoro katika Muungano. Anayesema uvunjwe ni haki yake kusema hivyo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nikumbushe, katika kitu chenye raha kweli kweli ni ndoa, lakini chenye shida kweli kweli ni ndoa. Takwimu za taasisi zinazofanya takwimu za uhalifu zinasema kwamba, idadi kubwa ya wanawake ambao wameolewa lakini ikatokea bahati mbaya wakauliwa kwa sehemu kubwa wanauliwa na wapenzi wao, yaani waliomo ndani ya ndoa *spouse* wao. Sasa unashangaa hawa watu waliomo kwenye ndoa wanafika wanauwana na ndoa ni taasisi ya mapenzi ya masikilizano, au kuna mtu sijui asimame aseme ama mimi ya kwangu bwana haina tatizo hata moja safi kabisa kila kitu, lakini nani atakayekuja akasema taasisi ya ndoa iuliwe haifai kwa sababu ina matatizo.

Sasa hayo ndio nasema ni mawazo ambayo mimi nadhani tuzingatie na ndio maana fursa imetolewa kwamba, umefanya juhudi yako yote imeshindikana ndio hiyo inakuja *last resort*. Lakini mimi naomba sana tuwaongoze watu wetu katika *process* hii, tutafute mambo ya msingi ambayo ni matatizo yapo yameelezwa, yameandikwa, wako wajasiri wa kusema lakini wako wajasiri mpaka walioandika, nadhani kwenye hili hakuna shida.

Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, ni suala la hoja hii ya Ada ya Bandari, mimi ninachotaka kukumbusha sitaki kwenda mbali kwa sababu hoja zimetolewa nyingi za kusema ubaya na uzuri wake au madhumuni yake. Lakini naomba nikumbushe tu, maana chombo chetu hiki kinaongozwa na Kanuni, kwa kweli Kanuni ndio roho ya chombo hiki bila ya Kanuni nadhani hakuna hodari wa kuendesha chombo hiki wala hodari wa kutoa hoja katika chombo hiki, uhodari unakuja kwa sababu ya taratibu madhubuti tulizojiwekea.

Mimi kabla ya kuingia humu nilikuwa nawaambia wenzangu siku zote kule nje kwamba, katika kitu ambacho mimi ninawasifu wanasiasa ni mahodari wa kufuata utaratibu mle ndani ya chombo chao, sijui wakitoka pale wanapata matatizo gani, lakini mle ndani ya chombo chao Baraza la Wawakilishi mahodari kweli kweli ukiteleza unaambiwa Kanuni, ukifanya hivi Utaratibu, ukiambiwa hivi Muongozo, wakitoka humu ndani sijui kunakuwa na tatizo gani lakini humu ndani *Alhamdulillah* kwa kweli. *(Kicheko)*

Sasa suala la hoja hii ya kuongezwa ada ya bandari naomba hili nilieleze vizuri kwa sababu tulifahamu tu msingi wake maamuzi anayo mwenyewe Mhe. Waziri hapa. Suala la ada ya bandari limo katika Sheria ya Ada ya Bandari ya mwaka 1999. Ile sheria chini ya kifungu cha 3 kifungu kidogo cha (4) imeweka jadweli na lile jadweli mwenye mamlaka chini ya kifungu 3(4) kubadilisha ni Mhe. Waziri anayeshughulikia Fedha na hii ndio kawaida takriban sheria nyingi za kodi hasa za ada. Inaeleza kwamba *substantive* mambo ya msingi, lakini inapokuja kwenye viwango hiyo kwa kawaida Baraza kwa sababu ya *nature* ya masuala ya ada basi kwa kawaida inampa waziri kubadilisha zile ada mara kwa mara. Nadhani mara nyingi kamati hapa zinalaumu kwamba viwango jamani Waheshimiwa Mawaziri wenye sekta zetu hamvibadilishi viko vile vile, sasa na sheria hii ni vile vile kwamba mamlaka yale yako katika mikono ya waziri kuweka ada kama zilivyo katika sheria nyengine.

Sasa jana au juzi tulipokuwa tunapitisha kwa hili la kuhusiana na bajeti Mhe. Waziri alipoleta Hoja ya Bajeti ya Serikali alieleza matumizi baadae akaeleza pesa atazipata pahala gani. Kwa hivyo, yale aliyoyaeleza atazipata pahala gani ile ilikuwa ni maelezo kwanza ndio nidhamu ya uwasilishaji wa bajeti na taratibu zake, lakini na pia kupata mchango wa Baraza hili. Tumejadili, tumeeleza kila mtu mwenye hoja yake, lakini mwisho hoja ya bajeti tukaipitisha, tulipoipitisha maana yake ni kwamba pamoja na kuwa wako watu ambao hawakuridhika, lakini kwa kuipitisha maana yake tumesema kwamba basi haya yaliyomo humu wewe endelea nayo.

Sasa kanuni zetu zinatuongoza chini ya kifungu cha 58(5) kwamba jambo ambalo Spika ameshawahoji Wajumbe na wakalitolea uamuzi Mjumbe haruhusiwi tena kulizungumza, sasa hoja ya bajeti ilishapitishwa kwa hivyo sasa tulipokuja huku kwenye *finance bill* na wakati wala hakuna hoja hiyo tena mana hivi viwango havizungumzwi kwenye *finance bill* hii hoja ya viwango ilikuja katika hoja ya bajeti, baada ya kuipitisha hata kama tuna *reservation* ndivyo ilivyo kwamba unaweza ukapitisha kitu una *reservation* zako, lakini ndio imeshapitishwa ile hoja kwa mujibu wa kanuni zetu huwezi tena suala lile. Mhe Mwenyekiti, labda naomba ninukuu.

Kifungu cha Kanuni cha 58(5) kinasema:

> "Hakuna Mjumbe yeyote atakayeruhusiwa kuzungumza suala ambalo Spika tayari ameshawahoji Wajumbe na uamuzi juu yake kutolewa"

Lakini sisi tukasema aa, ni vizuri Waheshimiwa Wajumbe wapumue serikali ipate kuwasikiliza, maana yale mamlaka yamo mikononi mwa waziri. Na mimi kwa sababu serikali ni sikivu ndio tukasema acha twende kidogo na huu mkorogo wa Kanuni imepitwa upande lakini tusikie tunapata faida ya kusikia. Waheshimiwa nashukuru wameeleza hoja zao na wameona kwamba labda hoja ya serikali.

Mimi nasema serikali yetu ni sikivu kuliko watu wanavyojua usikivu wake. Lakini na kwenye hili linaongozwa na waziri ambaye ni msikivu zaidi, naamini usikivu wake pengine utasaidia katika suala hili lakini hayo ni ya kwake yeye mwenyewe. Mimi nilitaka kutanabahisha tu suala la utaratibu kwa sababu ni vizuri sana tunapofanya mambo yetu tukenda ndani ya mstawi wa taratibu.

Mwisho kwa kumsaidia Mhe. Ismail Jussa lile suala alilosema ah, mbona haya mambo mengine yaliyotajwa zilitajwa sheria mbona humu kwenye mswada hazimo. Ni kwa msingi ule nilioeleza, ukitizama hizi sheria takriban zote zina majadweli na majadweli yale kazi ya kurekebisha au mamlaka ya kurekebisha tena takriban sheria zote ambazo zina ada yale masuala ya kurekebisha au yale ya ada hayo ni mamlaka ambayo amepewa waziri na ndio maana haku-*appear* katika huu mswada. Huu mswada una-*appear* katika vitu ambavyo ni vya msingi havimo katika jadweli lakini pengine Mhe. Waziri mwenyewe atakuja kufafanua vizuri zaidi.

Mimi nadhani ukija kwenye huu mswada ukiachia yale maudhui ambayo tumeyachangia sana yamesikika, lakini nadhani kimsingi dalili ni kwamba tumeyaunga mkono kwa asilimia mia moja na mimi naomba na ninawaomba sana Waheshimiwa tuupitishe ili tuweze kurekebisha mambo yetu mtupe fursa ili serikali iweze kuwatumikia watu wetu katika bajeti hii. Ahsante sana Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Kabla ya Mhe. Waziri hajasema niwaombe basi Wanadhimu wale wajumbe ambao wapo nje waanze kurudi ndani ili kusikia namna ya hoja zao zinavyojibiwa, lakini pamoja na kuendelea na utaratibu mwengine ambao umebakia mbele yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninataka nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai siku ya leo siku ya Ijumaa.

Vile vile ninataka nikupongeze wewe Mhe. Mwenyekiti kwa kukalia kiti. Vile vile ninataka niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe wote ambao wamechangia mswada ambao nimeuwasilisha jana. Kwa kuanza ninataka nimpongeze sana mwenyekiti wa wenyeviti, swahibu na mdogo wangu Mhe. Hamza Hassan Juma baada ya ule msiba wa Kenya wa ndugu yetu Saitoti, sijui sasa tutampa jina gani. Ninasubiri kikao kitakavyoamua jina jipya kwa uwasilishaji wake na michango yote iliyochangiwa na Wajumbe mswada wetu huu tokea jana hadi leo asubuhi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanzia ni vyema nikawatambua wale ambao waliochngia tokea jana hadi leo asubuhi. Wa kwanza nimpongeze:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe Asha Bakari Makame
4. Mhe. Hija Hassan Hija
5. Mhe. Salmin Awadh Salmin
6. Mhe. Abdalla Mohamed Ali
7. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
8. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
9. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
10. Mhe. Hassan Hamad Omar
11. Mhe. Assa Othman Hamad
12. Mhe. Saleh Nassor Juma
13. Mhe. Haji Faki Shaali
14. Mhe. Mwanasheria Mkuu

Mhe. Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi naomba na wao niwatambue:-

1. Mhe. Nassor Salim Ali

Mhe. Mwenyekiti, michango yote ilikuwa ni mizuri kama nilivyotangulia kusema na sina budi kuwashukuru wote ambao waliochangia.

Kwanza naanza na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati wa Wenyeviti. Ni kweli tulikubaliana makubaliano marekebisho yote yale tuyafanye na mwenzetu ameyaeleza hapa. Ninakubaliana yote yale marekebisho yote ambayo ameyaeleza. Mhe. Mwenyekiti, kwanza kulikuwa kuna hoja ambazo wenzetu

Wawakilishi wametushauri sana kupambana na wafanyakazi wadanganyifu wanaoikosesha serikali mapato.

Mimi ninasema Wawakilishi mukubali kuwa makamanda wadogo na mimi niwe kamanda mkuu kwa umoja wetu tupambane na hawa wanaoikosesha serikali mapato. Bila ya kujali mwanamke, mwanamme, itikadi ya siasa na itikadi ya dini.

Lengo letu haya mapato yatumike kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu. Kwa hivyo hili mimi ninakubaliana moja kwa moja. Tutasimama kidete kupambana na hawa wenzetu ambao wanaikosesha serikali yetu mapato.

Hoja ya pili Mhe. Mwenyekiti, ambayo imeibuka hatua gani tutazichukua pindipo wakala atabainika si muangalifu au muaminifu. Kwanza ninakubaliana na hoja hii lakini kuna sheria ya usimamizi wa kodi, sheria Na. 7 ya mwaka 2009 imetoa ufafanuzi wa kina. Kuna taratibu za faini mpaka za kifungo zipo, la msingi ambalo sisi tutapaswa sisi kulisimamia ni kuwa karibu na hawa wakala. Tusiwapururie mpaka kamba wameshaikata tukaanza kuwatafuta. Kila tukiwapa muda basi tuwe nao karibu ili tuweze kuona mwenendo wao ili muda mfupi tukiona mwenendo wao si mzuri tuweze kuchukua hatua.

Hili ninakubaliana nalo sana na tutakuwa karibu sana na hawa mawakala na wale wadanganyifu au wale ambao watakuwa si waaminifu tuweze kuchukua hatua katika kipindi kifupi badala ya kuwa mambo yameshaanza kuharibika kwa wingi zaidi.

Hoja nyengine ambayo iliyojitokeza Mhe. Mwenyekiti, wajumbe walitushauri basi Kanuni ziandaliwe haraka na ikiwezekana basi na wajumbe wapate kuziona na wao. Ninataka niseme tu kwamba Kanuni tayari zipo katika *draft*. Kwa sababu Kanuni hizi ndizo zitakazotusaidia hasa kutuongoza katika masuala yetu mbali mbali ya kodi na misamaha. Ninataka niwahakikishieni Waheshimiwa Wajumbe kwamba zitakapokamilika basi tutapata nafasi na sisi kuziona.

Hoja nyengine Mhe. Mwenyekiti, iliyoibuka ni serikali kuleta taarifa za misamaha Barazani. Nasema sina matatizo. Taarifa za misamaha za kila mwaka nitazileta hapa Barazani ili Baraza lione nani kapewa msamaha huo, ili lijue ni taasisi ipi iliyopewa msamaha huo na kiwango cha msamaha.

Kwa sababu msamaha ni kodi yetu ambayo tumeisamehe kwa manufaa ya maendeleo ya nchi yetu. Kwa hivyo mimi sioni sababu kwa nini nisikuleteeni mukaja mukaiona. Nitafanya jitihada hizo, na bahati nzuri sheria zinaniruhusu

kufanya hivyo, hakuna sheria inayonizuia. Nitazileta ndugu zanguni ili sote tuje tupeane maelekezo, kama Waziri wenu mutaona nimetoa msamaha mkubwa nielekezeni niupunguze nitaupunguza kwa sababu sheria tunazileta humu za kurekebisha hiyo misamaha. Kwa hivyo hili nitalitekeleza Mhe. Mwenyekiti, bila ya dharau na matatizo yoyote.

Hoja nyengine iliyoibuka na hii iliibuka kwa kweli ilikuwa ni kishindo kikubwa. Wawakilishi wetu kutosemea Bungeni. Hili ni letu wala si la Waziri wa Fedha. Tumewapeleka Wawakilishi watano; wanawake wawili na wanaume watatu. CUF wawili na CCM watatu.

Tunataka nini tena hapo. Kwa bahati nzuri wote wana midomo ya kusema. Sioni sababu kwa nini hoja zetu wazisemee humu waache kuzipeleka kule Bungeni. Hawa ni wetu. Bahati mbaya, ninasema ni bahati mbaya sheria inatuzuia kuwatoa, ukishakumtia umemtia. Lakini ingekuwa sheria inatupa uwezo wa kuwaondoa hawa badala ya kuwaingiza tungesema asiyetusemea tumtoeni. Kwa hivyo hawa ni wa kwetu, ndugu zetu. Sasa hivi ni kukaa nao jamani hoja zetu hizi mukazipigie debe kule. (*Makofi*).

Nilimuona Mhe. Assaa alipokuwa akijipapatua jana mpaka Mhe. Mwenyekiti, akavunja Kanuni za Baraza, maana tunaambiwa humu ndani huruhusiwi kuimba, yeye jana kaimba humu. Lakini hili ni letu. Mimi ninaelewa kwamba wenzetu wameghafilika tu lakini lengo lao lipo pale pale watatusidia kutusemea kwa zile hoja zetu ndani ya Bunge. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine ninataka nimshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu amenisaidia, hoja ya kudai haki zetu za muungano. Mwanasheria Mkuu ninakushukuru sana umenisaidia.

Jamani kelele tunapiga na sio kama hatupigi, barua sio kama hatuandiki hivyo, tunaandika mpaka mwisho tunaonekana kero. Nikinukuu mimi mpaka mwisho kwenye kikao chetu cha mwisho cha kupiga kelele kwa pamoja. Mhe. Haji Omar Kheir alithubutu kuwaambia wenzetu au kosa letu ni hii kuungana.

Sasa muone kwamba kelele tunapiga lakini pale aliposema Mwanasheria Mkuu, huyo unayempigia kelele anakusikiliza. Lakini ninataka nikuahidini waheshimiwa hatutasita kupiga kelele. Kuna siku wenzetu watatufahamu.

Lakini ninataka niseme tuna ule utaratibu wa *joint commission*. Katika ule utaratibu ule kuna madeni tunadaiana. Tutafika siku hili ni deni tu tutaliweka kwa sababu tumekubaliana wenzetu hawajatekeleza tutaliweka kama ni deni. Ni haki yetu. Mimi ninasema mtu mzima ukimuona analia ujue kuna jambo, hawezi mtu mzima akawa analia tu, ni lazima kuna jambo.

Humu ndani ya Baraza hili, sitaki nitaje kwa majina, tumelia ndani ya Baraza hili. Tukaulizana una nini wewe? Sasa mtu mzima unapomuona analia ujue kwamba lazima kuna jambo. Tutaendelea kufanya kelele na tutaendelea kujenga hoja, kwa sababu hoja zetu za madai yetu ni za msingi. (*Makofi*).

Mimi nina imani kubwa sana tutafika pahala hii itakuwa ni historia. Kwa hivyo nataka niseme tu tupeni nafasi ili tuyasimamie vizuri. Jana iliibuka hoja kwamba tusimamie pesa za rada. Sisi tulikuwa tumekaa masikio wazi tunasikiliza hasa mimi mwenzenu, kwa sababu mimi nilikuwa ni Naibu Waziri wa Ulinzi au mmesahau.

Ile rada ilinunuliwa kwa kutumia shughuli za muungano. Ulinzi ni masuala ya muungano ndio ikaekwa ile rada pale. Sasa ilipokuja kutokea la kutokea, wenzetu waliopata hizo pesa, Serikali ya Uingereza wakafanya maamuzi ya makusudi kusema jamani sasa hivi Tanzania tuirejeshee fedha zake.

Wamerejesha fedha lakini mambo mawili wametamka. La kwanza fedha hizo ziende kwenye shughuli za elimu. Elimu si masuala ya muungano na ile rada imenunuliwa kwa masuala ya muungano, tupeni za kwetu sasa asilimia 4.5 (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru sana Waziri wa Fedha Dk. William Mginywa tumemuelezea kwenye kikao chetu ameanza ku-*smile the face*. Tusipige kelele sisi tunajenga hoja zetu halafu kama kuna mtu anataka kuzifuta hizo hoja afute kwa hoja.

Mimi ninataka nikwambieni tu na mimi pesa za rada ninazitaka, mgao wangu ninautaka. Tutazifuatilia mpaka tuje tujibiwe kwa hoja tuone kwamba sisi hatustahiki. Kwa hivyo ninakuombeni Waheshimiwa tuaminini kwa hili.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine tuzidishe usimamizi katika ukusanyaji wa mapato. Hili nimelieleza kwa kina wakati ninajumuisha, tutaongeza usimamizi wetu tukisaidiana na Wajumbe wa Baraza lako Mhe. Mwenyekiti.

Ilikuja hoja nzito hapa utaratibu wa kukusanya kodi au fedha za viza ya Mhe. Salmin Awadh. Hoja yako ni sahihi kabisa wala haina utata na hata mimi nilikuwa ninahoji suala hili, unakwenda mtu na pasipoti anapigiwa muhuri tu, haionekani viza, risiti yenyewe inaandikwa kwa mkono tu, mtu anaweza akaandika au asiandike, hakuna pahala popote ambapo unaweza ukapata hiyo *record* halisi.

Suala hili tunalifanyia kazi. Lengo letu ni ku-*computerize* kila kitu. Mtalii akiingia picha yake itaingia kwenye kompyuta na risiti yake na visza yake

inatoka. Zuri zaidi viza ikitoka halafu na *information* ile ile inaingia katika benki ya PBZ. Hii tunaita ni *cheque and balance*. PBZ anaambiwa pato hilo limeshaingia la serikali na watu wa Uhamiaji wanaambiwa viza hiyo toeni.

Waheshimiwa Wajumbe turuhusuni muda mfupi tu tutarudi tena kuja kukupeni mkakati huo upo tayari, wala musiwe na wasi wasi. Mimi kila penye pesa ninaitaka iingie katika mfuko mkuu wa serikali.
Hoja nyengine ilikuwa ni utaratibu wa kuhifadhi mafuta ukoje, tuliulizwa hapa jana. Ninataka niseme tu kwamba hapa tunazungumzia mafuta ya biashara. Ukisema unataka kuweka mafuta kwa ajili ya biashara lazima ukapate kibali. Kwa sababu hiyo bidhaa yenyewe ndugu zangu ni bidhaa nyeti hii. Lazima tujue hapo unapoiweka, usalama wake kwa sababu hii ni bidhaa nyeti. Lakini leo una lita kumi upeleke kwenye gari yako imesimama pahala sio kitu tunachokizungumza, tunazungumzia kwa ajili ya biashara. Tujue hayo matangi na *storage* yako iko vipi.

Lakini kuna hoja ambayo imeibuliwa katika hili tungekuwa basi na kiwango. Nimeliangalia hilo, tutaangalia kiwango mahsusi kitakwenda kwenye Kanuni ili kila mmoja aweze kujua basi ukizidisha kiwango hiki lazima ukachuke kibali. (*Makofi*).

Hoja za Mhe. Jussa Mhe. Mwenyekiti, kwamba nimezungumza sheria mbali mbali kwenye hotuba lakini katika *finance bill* hazioni. Mwanasheria Mkuu ninadhani ametoa ufafanuzi mzuri.

Kwenye hotuba yangu nilikuwa ninataka nikwambieni tu waheshimiwa na huko ninarekebisha, lakini zaidi zipo kwenye Kanuni na *schedule*, kwa hivyo hazipo kwenye vifungu vikuu vya sheria mama. Kwa hivyo kule nilikuwa ninataka mulielewe kwamba kwenye Kanuni na *schedule* nazo vile vile nitazifanyia marekebisho ili kuweza kukidhi mahitaji yetu ya kodi mbali mbali pamoja na kulinda kodi zetu. Hili ninafikiri Mhe. Mwanasheria Mkuu ninakushukuru kwa ufafanuzi wako.

Mhe. Asha Bakari hapa nataka kuwa *specific* kwa kodi yako ya sigara na pombe. Nimefarajika sana dada yangu kodi hizi, nataka niseme tu kwamba wenzetu wa Serikali ya Muungano wamepandisha kwenye eneo hili. Zile ni mtiririko zinakuja zake mpaka huku. Kwa hivyo ndio maana tukaona sisi hapa tusipaguse tena na kwa kweli kuna kodi nyengine zinapandishwa tena kubwa kidogo.

Kuna baadhi ya sijui munaita vileo au vilevi, kwa sababu mimi sishiki hiyo, zimeongezewa mpaka shilingi mia tatu na tisini na tisa kwa lita moja na zile ninasema zitashuka mpaka huku. Kwa hivyo tumesema tusiziguse lakini

wangekuwa wenzetu hawajagusa tungeangalia jinsi gani ya kuweza kuzigusa huku, lakini tumeziacha kwa sababu kule zimeshaguswa.

Kulikuwa kuna hoja nyengine tutoze kodi kwenye eneo la visiwa vidogo, wazungu hawa watakapokwenda kule. Ninataka niseme tu kwamba hii ndio ile niliyoiongeza kutoka asilimia kumi na tano mpaka asimilia kumi na nane. Tayari nimeshaiongeza mpaka kwenye kisiwa kule kuna kodi ambayo wanaikusanya wenzetu wanaotembeza wageni na wanai-*remit* ZRB.

Kuna hoja nyengine Mhe. Mwenyekiti, ilizungumziwa kuhusu habari mabaya ya fedha za serikali. Hapa jana nilisema jana na nikawaomba Waheshimiwa Mawaziri tuwe karibu zaidi ili kusimamia zaidi, nikamuomba Mhe. Makamu vile vile. Lakini ninataka nikwambieni kuwa utaratibu wa Mhe. Rais sasa hivi kukutana na kila wizara katika kuleta mpango wake na matumizi kwa kila robo mwaka, kama Waziri hajitaki achezee.

Mimi ninataka nikwambieni Waheshimiwa Wajumbe utaratibu wa Waziri na Mhe. Rais, sio ule utaratibu wa babu na mjukuu wake, sijui kama munaujua huo. Babu na mjukuu, babu anafumba macho anamwambia mjukuu anamtizama kumbe kafumba macho, mjukuu anamuuliza babu umelala eeh! Babu anamjibu eeh! nimelala, mjukuu anamjibu tena babu basi na mimi babu ninalala eeh! Kumbe babu alikuwa anataka mjukuu alale kwa kumfumbia macho.

Lakini utaratibu wetu sisi na Mhe. Rais hautokuwa wa babu na mjukuu. Ukipeleka tu hapa ukafikiria unataka kumdanganya Rais kwa Bango lako Kitita si rahisi. Ni Rais yupi wa kudanganywa. Dk. Shein si rahisi. Mimi ninataka niseme Waziri anayetaka kufanya stori ya babu na mjuu kwa Dk. Shein shauri yake mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, ninafikiri nimezizungumza hoja zote, sijui kama kuna hoja ambayo nimeibakisha, ipo moja. Hoja ya bandari na hii itakuwa ni hoja yangu ya mwisho.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninataka niseme tu kwamba Mwenyekiti wa Wenyeviti tunafahamiana vizuri sana, na kweli kweli tulilizungumza kwa kina suala hili kwenye kamati ya wenyeviti.

Nakumbuka siku hiyo, sijui kama alikuwa kuna mwenyekiti aliyekuwa hakuwepo, sijui kuna Waziri mwengine anayekutana na Kamati ya Wenyeviti isipokuwa mimi. Ninadhani hii kamati imeundwa kwa ajili yangu mimi.

Tulilizungumza kwa kina juu ya suala hili. Baadae Waheshimiwa hawa wenyeviti kwa umoja wao waliniomba kwamba hii kodi kama haiwezi kuondoshwa basi muipunguze. Hoja yangu ya msingi niliwaomba waje nalo hapa ili Baraza hili ndio lenye dhamana ya kufanya hiyo shughuli.

Nimesikiliza kilio kikubwa sana cha Waheshimiwa Wawakilishi kwa umoja wetu, lakini vile vile ninataka tusisahau madhumuni ya hoja hii bado yatabakia pale pale kwamba tuna tatizo la madawati. Na ni dhahiri kwamba kuna haja ya kuwapatia madawati vijana wetu lakini limesemwa na wengi. Karibu wajumbe wote wamelisema.

Binadamu anapotemewa mate na wengi mwishowe anaroa. Leo nimevaa vazi hili musinitemee mate, lakini mimi nimefurahi. Wengi hapa wamezungumza hapa kwamba serikali ni sikivu na serikali inaongozwa na Dk. Shein ni Rais wetu na msikivu. Kama aliweza kuondoa Dk. Shein shilingi elfu arobaini za akinamama. Leo mimi Omar Yussuf Mzee kwa uongozi wa Dk. Shein nang'ang'ana na shilingi elfu moja.

Kuna mzee alimchukua mwanawe siku ya sikukuu, yule mtoto akawa baba katika kujipigapiga hana vitu, kakosa pesa za viatu. Mtoto alilia sana kwa nini mimi viatu vipya sina, ninakwenda miguu chini, juu nimevaa. Baba katika kumpakia ndio wanakwenda katika viwanja vya sikukuu akapita njiani akamkuta mtoto mwenziwe maskini ana mguu mmoja kavaa kiatu kimoja, akamwambia mwanangu unamuona yule, yule hata ukimpa viatu viwili atakivaa kiatu kimoja tu. Wewe una miguu, mtoto kilio kikapungua.

Kwenda naye tena wakakutana tena mtoto mwengine hana miguu yote miwili. Akamwambia mwanangu unamuona yule hana ukimpa hivyo viatu hawezi kuvivaa hata kimoja, mtoto akanyamaza kulia. Lakini juu ya jitihada zangu za kukuelezeni kodi hii ninavyotaka kuitumia wazee nyinyi bado munalia, ukimuona mtu mzima analia kuna jambo. Mhe. Mwenyekiti, basi ninataka niseme kwamba kodi hii tumeiondoa. lakini Mhe. Mwenyekiti, kodi niliyoiondoa ni ile iliyoliliwa sana ya Unguja na Pemba. *(Makofi).*

Sasa kwa heshima na taadhima Mhe. Mwenyekiti, naomba nikakae tupitishe mswada wetu kiulaini, twende tukaswali Ijumaa tumuombe Mwenyezi Mungu mambo yetu yawe mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Leo kweli, mpaka *backbenchers* wamenyanyuka wote kwa ajili ya kupitisha hoja. Sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji basi wale

wanaoafiki hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mikono. Wasioafiki. Walioafiki wameshinda Ahsante.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama kamati ya kutunga sheria ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Kifungu cha 1	Jina Fupi na Kuanza Kutumika.

SEHEMU YA PILI
MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI NAMBARI 4 YA MWAKA 1998

Kifungu cha 2	Kusomwa.
Kifungu cha 3	Marekebisho ya Kifungu cha 2 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 4	Marekebisho ya Kifungu cha 7
Kifungu cha 5	Marekebisho ya Kifungu cha 13
Kifungu cha 6	Marekebisho ya Kifungu cha 14
Kifungu cha 7	Marekebisho ya Kifungu cha 16 pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 8	Marekebisho ya Kifungu cha 66

SHEMU YA TATU
MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA STEMPU NAMBARI 6 YA MWAKA 1996

Kifungu cha 9	Kusomwa.

Kifungu cha 10 Marekebisho ya Kifungu cha 2

Kifungu cha 11 Marekebisho ya Kifungu cha 3

Kifungu cha 12 Marekebisho ya Kifungu cha 12

Kifungu cha 13 Marekebisho ya Kifungu cha 13(B)

Kifungu cha 14 Marekebisho ya Kifungu cha 15

SEHEMU YA NNE
MAREKEBISHO YA SHERIA ZA KODI ZA HOTELI
NAMBARI MOJA YA MWAKA 1995

Kifungu cha 15 Kusomwa.
Kifungu cha 16 Marekebisho ya Kifungu cha 2
Kifungu cha 17 Marekebisho ya Kifungu cha 3

SEHEMU YA TANO
MAREKEBISHO YA SHERIA YA KUTOZA KODI YA MAFUTA
NAMBARI 7 YA MWAKA 2001

Kifungu cha 18 Kusomwa.

Kifungu cha 19 Marekebisho ya Kifungu cha 15(A)

SEHEMU YA SITA
MAREKEBISHO YA SHERIA YA ADA YA BANDARI
NAMBARI 2 YA MWAKA 1999

Kifungu cha 20 Kusomwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nataka nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nikazungumzia kidogo kuhusu kifungu cha 20. Mhe. Mwenyekiti, madhumuni ya kusimama ilikuwa zaidi kumshukuru sana Mhe. Waziri, kama tulivyosema ni mtu ambaye ni msikivu na ni mtu ambaye anajali maslahi ya watu wa Zanzibar. Kwa kuwa aliwahi kuwa mbunge wa jimbo. Kwa hivyo anajua ni namna gani wananchi walivyokuwa na matatizo katika maisha yao.

Lakini kubwa Mhe. Mwenyekiti, nililotaka kusisitiza hapa ni kwamba kuna ushauri mwingi ambao ulitolewa kwa baadhi ya kodi ambao mpaka sasa hivi serikali haizikusanyi. Kwa hivyo, mimi nadhani tungemuomba Mhe. Waziri

akajitahidi kuzisimamia kodi zile ili zikaweza kuziba pengo ya ile ada ya shilingi 1,000/- ambayo ameikubali na namshukuru Mhe. Rais ambaye wameshauriana na ameikubali.

Mhe. Mwenyekiti, ada zenyewe nilikuwa najaribu kuangalia zaidi kuna nyumba ambazo wananchi wamewakodisha hasa wageni, na nyumba hizi hazikusanywi kodi ya serikali, na nyumba hizi nyingi ziko katika sehemu za pwani, na maeneo mfano kama Mazizini na maeneo mengine. Kwa hivyo, hii kodi itaweza kusaidia serikali.

Vile vile kuna ukataji mkubwa sana wa miti hapa Zanzibar sasa hivi. Kuna ada ambayo inatakiwa kukusanywa ya shilingi 3,000/- kwa kila mti unaokatwa. Ada hii Mhe. Mwenyekiti, haikusanywi na kama inakusanywa basi haikusanywi ipasavyo. Nadhani Mhe. Waziri lile pengo ambalo tulilikosa katika ada hii ya shilingi 1,000/- nafikiri tunaweza tukalikusanya katika sehemu nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo nia yangu ya kusimama zaidi ni kumshukuru Mhe. Waziri lakini pamoja na serikali yetu kwa usikivu wa kauli ya wananchi wao, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 20	Kusomwa.
Kifungu cha 21	Marekebisho ya Kifungu cha 2
Kifungu cha 22	Marekebisho ya Kifungu cha 3(A)
Kifungu cha 23	Marekebisho ya Kifungu cha 14

SEHEMU YA SABA
MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI WA KODI NAMBARI 7 YA MWAKA 2009

Kifungu cha 24	Kusomwa.
Kifungu cha 25	Marekebisho ya Kifungu cha 2
Kifungu cha 26	Marekebisho ya Kifungu cha 45 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 27	Marekebisho ya Kifungu cha 57

SEHEMU YA NANE
MAREKEBISHO YA SHERIA YA BODI YA MAPATO YA ZANZIBAR NAMBARI 7 YA MWAKA 1996

Kifungu cha 28	Kusomwa.
Kifungu cha 29	Marekebisho ya Kifungu cha 5
Kifungu cha 30	Marekebisho ya Kifungu cha 9

SEHEMU YA TISA
MAREKEBISHO YA SHERIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII NAMBARI 2 YA MWAKA 2005

Kifungu cha 31	Kusomwa.
Kifungu cha 32	Marekebisho ya Kifungu cha 27

SEHEMU YA KUMI
SHERIA YA MAFUNZO YA AMALI NAMBARI 8 YA MWAKA 2006

Kifungu cha 33	Kusomwa.
Kifungu cha 34	Marekebisho ya Kifungu cha 15

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
MAREKEBISHO YA SHERIA YA UKUZAJI VITEGA UCHUMI NAMBARI 11 YA MWAKA 2004

Kifungu cha 35	Kusomwa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 36	Marekebisho ya Kifungu cha 19 pamoja na marekebisho yake.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu, na kuukubali. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji. Wale wanaokubali hoja ya Mhe. Waziri wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. Ahsante. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Fedha na Usimamizi wa Mapato 2012

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Fedha, Usimamizi wa Mapato ya Mwaka 2012, usomwe kwa mara ya pili.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Serikali ulisomwa mara ya pili na kipitishwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa napenda kuchukua fursa hii kukushukuruni sana, kwa namna ambavyo tumeweza kushirikiana pamoja, hadi tukaweza kufikia hapa ikawa kazi yetu kwa ujumla wake tumemaliza kwa siku ya leo. *Inshaallah* nichukuwe basi fursa hii kukushukuruni tena kwa mara nyengine. Lakini pia kuweza kuakhirisha Baraza hili tukufu hadi siku ya Jumatatu saa 3:00 za asubuhi, tarehe 25/06/2012.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaakhirisha nawaomba wale wanachama wote wa Chama cha Mapinduzi, ikimaliza tu shughuli hii wabakie hapa; ahsanteni sana. Naomba kuakhirisha.

(Saa 5:10 asubuhi Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 25/06/2012 saa 3:00 asubuhi)